www.vpo.go.tz

# OFISI YA MAKAMU WA RAIS

MUUNGANO NA MAZINGIRA TOLEO NA. 30 DESEMBA, 2019

# Serikali yafanyia marekebisho Kanuni za Udhibiti wa Taka Hatarishi za mwaka 2019



Uk. 2

Jarida hili limetolewa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini - S.L.P. 2502, Dodoma

ofisi ya makamu wa rais

ofisi ya makamu wa rais

@vpo_tanzania





# Serikali yafanyia marekebisho Kanuni za Udhibiti wa Taka Hatarishi za 2019



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira Mhe. George Simbachawene amesema Ofisi yake imefanya Marekebisho ya Kanuni na kutunga Kanuni Mpya za Udhibiti na Usimamizi wa Taka Hatarishi za mwaka 2009, Kanuni za Ada na Tozo za Usimamizi wa Mazingira za Mwaka 2008 na marekebisho yake ya mwaka 2016 na 2018, pamoja na Kuandaa Kanuni mpya za Udhibiti na Usimamizi wa Taka za Kielektroniki za Mwaka 2019

Simbachawene amesema hayo ofisini kwake jijini Dodoma ambapo aliwataka baadhi ya watu wanaojihusisha na vitendo vya kuhujumu miundombinu ya umma na ya watu binafsi ili kwenda kuuza kama chuma chakavu kuacha mara moja.

Alisema hatua iliyochukuliwa na Ofisi hiyo ya kufanya marekebisho katika kanuni hizi na kuweka mfumo bora wa kisheria wa kusimamia taka hatarishi inalenga sio tu kuhakikisha kuwa mazingira yanalindwa na kusimamiwa bali pia miundombinu ya nchi inalindwa ipasavyo.

Aidha waziri huyo aliwataka baadhi ya wanaofanya biashara hiyo huku wakikwepa kulipa kodi stahiki kuacha udanganyifu huo kwani sasa Serikali imeweka mfumo wa kiutawala, kisheria na kikanuni ambao sio rahisi kufanya udanganyifu huo tena bila kugundulika.

Aliongeza kuwa katika kuboresha usimamizi wa mazingira, Ofisi imefanya marekebisho ya Kanuni mbalimbali pamoja na kutunga Kanuni Mpya zikiwemo za Udhibiti na Usimamizi wa Taka Hatarishi za mwaka 2009.

Kanuni zingine ni za Ada na Tozo za Usimamizi wa Mazingira za Mwaka 2008 na marekebisho yake ya mwaka 2016 na 2018, pamoja na Kuandaa Kanuni mpya za Udhibiti na Usimamizi wa Taka za Kielektroniki za Mwaka 2019.

Simbachawene alifafanua kanuni mpya za mwaka 2019, zimeainisha aina ya shughuli za usimamizi wa taka hatarishi ambazo zinapaswa kuwa na kibali cha Waziri mwenye dhamana ya Mazingira akitaja shughuli zinazopaswa kuombewa kibali ndani ya nchi ni kukusanya, kutunza, kusafirisha na kumiliki au kuendesha mtambo wa usimamizi wa taka hatarishi.

Aidha, shughuli za usafirishaji nje ya nchi, kuingiza au kupitisha nchini taka hatarishi zinapaswa kuombewa kibali ambacho pia hutolewa na Waziri husika na zimeelekeza shehena yoyote ya taka hatarishi itakayoingizwa au kupitishwa nchini bila kufuata masharti ya Kanuni hizi, itachukuliwa kuwa ni usafirishaji haramu wa taka hatarishi na zinapaswa kurejeshwa katika nchi zilikotoka kwa gharama za msafirishaji.

Waziri Simbachawene aliongeza kuwa kanuni hizi zimeweka adhabu kali zaidi kwa makosa ya kutokuwa na kibali cha kusimamia taka hatarishi nchini zikiwemo faini kuanzia sh. milioni tano hadi bilioni 10 au kifungo kisichozidi miaka 12 au vyote kwa pamoja.

# Tanzania yasihi Mataifa yachukue hatua kushughulikia mabadiliko ya tabianchi




Tanzania imetoa wito kwa jumuiya ya kimataifa kuchukua hatua za haraka na za pamoja kushughulikia suala la mabadiliko ya tabianchi na athari zake.

Hayo yalisemwa na Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais Mhe. Mussa Sima katika mkutano wa 25 wa Mawaziri wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi unaondelea Madrid nchini Hispania.

Aliwataka wajumbe wanaoshiriki katika mkutano huo kuendelea kuchukua hatuamahsusi za kushughulikia changamoto za mabadiliko ya tabianchi.

"Tunahitaji kuendeleza kasi ya kushughulikia mabadiliko ya tabianchi kwa kubainisha malengo mahususi ya kupunguza tatizo hilo kwa kuchukua hatua zote muhi6 mu zinazohitajika" Sima alisisitiza.

Aidha ameeleza kuwa athari za mabadiliko ya tabianchi tayari zimeathiri Tanzania kupitia matukio makubwa ya hali ya hewa ikiwemo mvua nyingi na kuongeza kwa joto ambavyo vinasababisha mafuriko na kusambaa kwa magonjwa ambukizi, upotevu wa mali na maisha ya wanadamu na uharibifu wa miundombinu ya barabara na madaraja katika maeneo mengi ya nchi.

Pia, Naibu Waziri alibainisha kuwa, kwa mujibu wa taarifa za Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), Oktaba mwaka huu imekuwa na mvua nyingi ulikinganisha na kipindi kingine kama hicho kwa karibu muongo mmoja ulio pita na kuathiri sekta zote muhimu, kama vile kilimo, afya, uvuvi, mifugo, maji na afya hivyo kuongeza kwa magonjwa yakiwemo dengue na malaria.

Katika hatua nyingine Naibu Waziri Sima alibainisha kuwa Serikali ya Tanzania chini ya Rais Dkt John Pombe Magufuli, imekuwa ikichukua hatua thabiti ambazo zinachangia katika kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi na ongezeko la gesijoto licha ya ukweli kuwa haikuchangia katika chanzo cha tatizo hilo.

Aliuarifu mkutano huo kuwa Tanzania imenunua rada mbili zitakazotumiwa na TMA kwa lengo la kuongeza ufanisi wa utabiri hali ya hewa na majanga yatokanayo na athari za mabadiliko ya tabianchi, inaendela kupanua na kujenga mtandao wa barabara za mabasi ya mwendo wa haraka katika jiji la Dar es Salaam; inajenga reli ya viwango vya kimataifa (SGR) na kujenga bwabwa la Mwalimu Nyerere ambalo litazalisha kiasi cha 2115MW.

"Utekelezaji wa miradi hii sio tu unachochea mandeleo ya taifa na ukuaji wa uchumi, bali unachangia pia katika upunguzaji wa gesijoto ambazo zinasabaisha ongezo la joto la dunia ambalo husabaisha mabadiliko ya tabianchi" Sima aliongezea.

Pamoja na hayo, Sima aliuarifu mkutano wa Madrid kuwa, Tanzania imedhamiria kuendelea kuongeza maeneo yanayonyonya gesijoto na kutunza uoto wa asili kwa kuwa na eneo la misitu lenye ekari takiriban milioni 48, kuendelea kuongeza eneo ambalo limehifadhiwa kwa kuongeza idadi ya hifadhi za taifa na kuendelea na kampeni ya upandaji miti nchi nzima.

# Balozi Sokoine:Mifumo bora ya ikolojia husaidia kuhimili mabadiliko ya tabianchi



Mifumo ikolojia yenye afya ndio inaweza kutupatia huduma za uhakika kama chakula, maji safi na salama, kutuepusha na magonjwa, mafuriko, uharibifu wa ardhi na wakati huo huo kutuwezesha kuhimili athari zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi.

Hayo yalisemwa na Naibu Katibu kuu Ofisi ya Makamu wa Rais Balozi Joseph Sokoine ambaye alikua mgeni rasmi katika ufunguzi wa warsha ya mafunzo kuhusu kuhimili mabadiliko ya tabia Nchi kwa kutumia mifumo ya ikolojia iliyofanyika katika ukumbi wa chuo cha Mipango jijini Dodoma.

Alisema kuwa Kukosekana kwa huduma hizo kutapelekea kushindwa kufikia milenia (Sustainable Development Goals). Hivyo mradi huu umekuja wakati muafaka wakati pia Serikali ikiendelea kukuza uchumi katika njia endelevu.

"Kama mnavyo fahamu mabadiliko ya tabianchi yameleta athari mbalimbali kwenye mazingira yetu hapa nchini. Kati ya madhara hayo ni kuharibika kwa kanda za Ikolojia Kilimo (Agro Ecolojical Zones) ambazo kwa mujibu wa tafiti kanda hizi ziko saba. Tafiti zinaonyesha kwamba ni rahisi kuhimili (Adaptation) kuliko kukabili (Mitigation)". Alifafanua Balozi Sokoine.

Akimkaribisha Mgeni Rasmi Kaimu Mkurugenzi wa Mazingira Bwana Fara ja Ngerageza alisema kuwa warsha hiyo itawawezesha washiriki kufahamu zaidi kuhusiana na kuhimili mabadiliko ya tabia nchi kwa kutumia mifumo ya ikolojia iliyopo vijijini.

Warsha hiyo ya mafunzo ya siku tatu imeandaliwa na Ofisi ya Makamu wa Rais kupitia mradi wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi kwa kutumia mifumo ya ikolojia vijini (EBARR).

Mradi huu unatekelezwa na Ofisi ya Makamu wa Rais. Warsha hiyoimehudhuriwa na Washiriki kutoka Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali, ilifanyika katika ukumbi wa Mikutano wa chuo cha Mipango jijini Dodoma.

# MATUKIO KATIKA PICHA



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akisalimiana na Rais Dkt. John Magufuli wakati wa sherehe za miaka 58 ya Uhuru wa Tanganyika katika Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.*



*Waziri wa Nchi OMR (Muungano na Mazingira) Mhe. George Simbachawene akibadilishana mawazo na wabunge wa Pemba alipokagua miradi ya Mfuko wa Jimbo kisiwani humo.*



*Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Mhandisi Joseph Malongo akipokea tuzo ya uandaaji bora wa taarifa za hesabu kwa mwaka 2018 kutoka kwa Mhasibu Mkuu wa Ofisi hiyo Pascal Karomba.*



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Suluhu Hassan akiwa na Msanii wa Kikundi cha Ngoma ya Matoigaa Charoo cha Ukara, Ukerewe, Mwanza Goabth Bwere baada ya kuzindua majengo mapya ya Kituo cha Afya.*




*Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Mussa Sima (wa pili kulia) akifuatilia majadiliano katika Mkutano wa Mashauriano kati ya Serikali, Wawekezaji na Wafanyabiashara wa Mkoa wa Morogoro.*



*Waziri wa Nchi OMR (Muungano na Mazingira) Mhe. George Simbachawene akisalimiana na sehemu ya watumishi wa Ofisi hiyo Zanzibar alipowatembelea.*

# Serikali yasisitiza haitaruhusu mifuko mbadala isiyokidhi vigezo vya ubora

Serikali imesema kamwe haitaruhusu uzalishaji, uingizaji na matumizi ya mifuko mbadala aina ya *Non-Woven* isiyokidhi viwango vya 70 *Gram Per Square Metre* (GSM) kutumika nchini.

Hayo yamesemwa na Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais Mussa Sima (pichani) katika Mkutano wa Mashauriano baina ya Serikali, Wafanyabiashara na Wawekezaji uliolenga kusikiliza na kutatua changamoto zao, Mkutano uliofanyika katika ukumbi wa Chuo cha Uuguzi Kibaha mkoa wa Pwani.

Awali akiwasilisha taarifa ya Mkoa, Mkuu wa Mkoa wa Pwani Mhandisi Evarist Ndikilo amesema kuwa kumekuwa na uchelewashaji wa utoaji wa vibali vya kuingiza mifuko mbadala nchini kutoka Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira hali ambayo inaleta vikwazo kwa wafanyabiashara na wawekezaji.

Akitoa ufafanuzi wa ucheleweshaji wa vibali hivyo Mhe. Sima amesema kuwa Serikali imepiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki nchini tangu Juni Mosi 2019 na kutoa fursa kwa wakezaji kuagiza na kuzalisha mifuko mbadala ili kukidhi soko la ndani.

Hata hivyo changamoto imejitokeza kwa wafanyabiashara wasio waaminifu kutaka kuingiza mifuko isiyokidhi viwango aina ya *Non-Woven*.

"Kumeanza kujitokeza uvunjifu wa sheria katika uzalishaji na uingizaji wa mifuko mbadala aina ya *non-woven*. Shirika la Viwango Tanzania (TBS) limeweka vigezo vya mifuko mbadala aina ya *non-woven* inayoweza kutumika nchini ikiwa ni pamoja na Uzito usiopungua GSM 70 (Gram per Square Metre), iweze kurejelezwa, Ioneshe uwezo wa kubeba, anuani ya mzalishaji na iwe imethibishwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS)" Sima alifafanua.

Alisisitiza busara itumike katika kumaliza mgogoro uliopo baina ya mfanyabiashara aliyeagiza bidhaa hiyo huo bila kuathiri upande wowote kwa kutoa mapendekezo kwa mfanyabiashara mwenye mzigo husika kuurejereza ama kuusafirisha nje ya chini ya uangalizi maalumu na kuagiza Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) na Shirika la Viwango nchini (TBS) kumaliza suala hilo mapema iwezekanavyo.



Katika hatua nyingine Naibu Waziri Sima amesema kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais imefanya mapitio ya Kanuni za Taka Hatarishi za mwaka 2009 na kutunga Kanuni mpya ya mwaka 2019 ambazo zimezingatia Mkataba wa Basel yaani *Basel Convention for trans-boundary Movement of Hazadous Waste* ambao Tanzania imeridhia baada ya awali biashara hiyo hairatibiwi ipasavyo.

"Kwa mujibu wa Mkataba huu, mfanyabiashara anapotaka kuingiza Hazadous Waster ikiwemo chuma chakavu pamoja na masharti mengine ni lazima nchi ambapo chuma chakavu kinatoka kupata kibali cha Serikali ya nchi husika ili kuthibitisha kuwa nchi hiyo imeruhusu usafirishaji huo" Sima alisisitiza.

Amefafanua kuwa malighafi inayotumika na Viwanda vya ndani imekuwa ikipelekwa nje, hivyo Serikali imeweka masharti magumu kwa lengo la kulinda viwanda vya ndani na kuruhusu kusafirishwa kwa malighafi ambayo haitumiki hapa nchini.

Naibu Waziri Sima aliwahimiza wawekezaji kuwekeza katika Mkoa wa Pwani na kutumia nishati ya gesi kwa wingi. "Ni viwanda 48 tu nchi nzima ndio vinatumia nishati ya gesi, wawekezaji wekeni nia ya matumizi ya Gesi ili TPDC waweke miundombinu stahiki, nawasihi ndugu zangu tulinde mazingira yetu".

Siku ya pili ya Mkutano wa Mashauriano baina ya Serikali, Wafanyabiashara na Wawekezaji ambao ulifanyika katika ukumbi wa Chuo cha Uuguzi Kibaha mkoa wa Pwani na kuhudhuriwa na washiriki kutoka Wilaya zote za Mkoa wa Pwani.

# Waziri Simbachawene awataka watendaji kuzingatia sheria wanaposimamia miradi

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. George Simbachawene amewataka watendaji wa Serikali wanaosimamia miradi mbalimbali ya maendeleo kuzingatia sheria wanapotekeleza shughuli zao.

Simbachawene ametoa kauli hiyo wilayani Chakechake, Pemba wakati wa majumuisho ya ziara yake ya kikazi ya kukagua miradi ya Mfuko wa Jimbo katika wilaya za Wete na Chakechake kisiwani Pemba.

Alisema kuwa Katika kuhakiksha mfuko unatekelezwa vizuri watendaji hao wana wajibu wa kuhakikisha wanashiriki kikamilifu katika hatua zote za utekelezaji wa miradi ili mwishoni waweze kuandika taarifa.

Akizungumza na wabunge wa majimbo yaliyopo katika wilaya hizo pamoja na watendaji hao alibainisha kuwa nafasi ya mbunge na kamati inayosimamia mradi kupitia Mfuko wa Jimbo ni kubwa na wanapaswa kufanya kazi hadi kukamilika kwake.

"Wajibu wa kamati unaendelea hadi mradi ukamilike kwani baadaye mtatakiwa kuandika ripoti ya nini kimefanyika tangu mwanzo wa mradi hivyo kukataa kushirikiana na mbunge hakuna tija ni kinyume cha utaratibu na sheria na pia mbunge anapaswa



***Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. George Simbachawene akizungumza wakati wa kikao cha majumuisho ya ziara wilayani Chakechake. Kushoto ni Mbunge wa Mtambile, Mhe. Masoud Abdallah Salim.***

kusimamia mradi kuona kama kuna value for money," alisisitiza.

Kwa upande wake Kaimu Mkurugenzi wa Muungano Ofisi ya Makamu wa Rais, Lupi Mwaikambo alisema ipo haja ya kukutana na wakurugenzi wa wilaya na mabaraza ya miji kwani ndio wanadaiwa kuwa kikwazo katika miradi hiyo.

Alisema ni muhimu wakurugenzi hao wawe na ushirikiano mkubwa na watendaji wao ambao ni maafisa mipango kwani ndio wanasimamia ya maendeleo washirikiane na wataalamu.

Awali wakitoa maoni yao kwa waziri baadhi ya wabunge akiwemo Maida Hamed Abdallah wa Viti Maalumu Mkoa wa Kaskazi- wanashirikishwa katika kamati za miradi ndani ya majimbo pamoja na kuwa wao hawana mufuko wa jimbo.

Walisema kuwa kutokana na wao kutokuwa sehemu ya kamati inakuwa ni jambo gumu kuweza kulitolea ufafanuzi wa namna gani fedha za mfuko zimetumika kwakuwa wanakosa taarifa muhimu.

Miradi aliyotembelea Simbachawene ni mradi wa skuli ya maandalizi Kangagani na mradi wa maji safi na salama Wingwi Mjazana iliyopo Wilaya Wete.

Pia alitembelea miradi ya skuli ya Vikungani na mradi wa umeme wa Pujini iliyopo Wilaya ya Chakechake.

# Sima: Serikali kurahisisha mazingira ya uwekezaji nchini




Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Mussa Sima amesema Serikali imefanya mapitio ya Kanuni ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira ili kurahisha uwekezaji nchini.

Akizungumza na Wafanyabiashara na Wawekezaji katika Mkutano wa Mashauriano baina yao na Serikali katika ukumbi wa Hoteli ya Glonency mkoani Morogoro, Naibu Waziri Sima amesema gharama za kulipia vibali zimepungua na idadi ya siku pia imepungua kutoka siku 145 mpaka siku 95 hivi sasa

"Ndugu zangu marekebisho haya yote yanayofanywa na Serikali, yanalenga kurahisisha mchakato wa uwekezaji hapa nchini, Mfano awali gharama kwa vituo vya mafuta zilikuwa zaidi ya Milioni kumi na kwa sasa gharama hizi zimepungua hadi kufikia Milioni Nne na nyingine Milioni mbili" Sima alisisitiza.

Katika hatua nyingine Naibu Waziri Sima, amesema Ofisi yake inaandaa Kanuni za Wataalamu Elekezi wa Mazingira ili kurahisisha uwekezaji kwa kuwa miradi yote ni lazima ipate cheti kutoka Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC). "Tangu tumefanya mapitio ya Kanuni zetu, malalamiko kutoka kwa wawekezaji yamepungua kwa kiasi kikubwa sana" Sima alisisitiza

Hata hivyo Naibu Waziri Sima amewakumbusha washiriki wa Kikao hicho kuwa Mabadiliko ya tabianchi ni tatizo kubwa duniani, na kutoa rai kwa umma wa watanzania kupanda miti kwa wingi kupunguza athari za mabadiliko ya Tabianchi. Amewaagiza wawekezaji hasa wenye Viwanda kuhakikisha wanaanzisha vitalu vya miche katika maeneo yao na kusisitiza kuwa ukaguzi wa masuala ya Mazingira katika maeneo yao utaanzia hapo

Mkutano huu wa Mashauriano baina ya Serikali, Wafanyabiashara na Wawekezaji ulilenga kusikiliza na kutatua changamoto zao ulifanyika Morogoro ukihusisha Mawaziri na Manaibu Waziri 13.

## TAARIFA KWA UMMA KUHUSU KANUNI ZA UDHIBITI NA USIMAMIZI WA TAKA HATARISHI ZA MWAKA 2019, KANUNI ZA UDHIBITI NA USIMAMIZI WA TAKA ZA KIELEKTRONIKI ZA MWAKA 2019 NA KANUNI ZA ADA NA TOZO ZA USIMAMIZI WA MAZINGIRA ZA MWAKA 2019

**Ndugu Wananchi,**

Ofisi ya Makamu wa Rais imepewa Mamlaka ya kusimamia na kuratibu masuala yote yanayohusu mazingira nchini kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 na Kanuni zake. Aidha, usimamizi na udhibiti wa taka zenye madhara umebainishwa kwenye Vifungu vya 133 -139 vya Sheria hii.

Taka hatarishi au taka zenye madhara ni pamoja na vyuma chakavu, taka za kieletroniki, dutu hatarishi, mafuta machafu, taka za hospitali, betri zilizotumika na aina ya taka zote zinazotoka migodini. Taka hizi hatarishi zinaweza kusababisha athari kwa afya ya binadamu, viumbe hai na mazingira. Ili kuzuia na kudhibiti athari zitokanazo na taka zenye madhara, mfumo mahsusi unaofanya kazi kwa ufanisi wa kudhibiti taka hizi unapaswa ufuatwe kama ulivyobainishwa kwenye Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004.

Katika kuboresha usimamizi wa Mazingira, Ofisi imefanya Marekebisho ya Kanuni mbalimbali pamoja na kutunga Kanuni Mpya.

Mojawapo ya Kanuni zilizofanyiwa mapitio na kufanyiwa marekebisho ni Kanuni za Udhibiti na Usimamizi wa Taka Hatarishi za mwaka 2009; Kanuni za Ada na Tozo za Usimamizi wa Mazingira za Mwaka 2008 na marekebisho yake ya mwaka 2016 na 2018, pamoja na Kuandaa Kanuni mpya za Udhibiti na Usimamizi wa Taka za Kielektroniki za Mwaka 2019.

Kanuni mpya za Usimamizi wa Taka Hatarishi za mwaka 2019 [*The Environmental Management (Hazardous Waste Control and Management) Regulations, 2019*]; zimezingatia masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kama ifuatavyo:

Kifungu cha 133(1) na (3) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004, kinampa mamlaka Waziri mwenye dhamana ya mazingira kutoa vibali vya kuingiza, kusafirisha nje ya nchi, kusafirisha ndani ya nchi au kupitisha taka hatarishi nchini. Hata hivyo, Kanuni za mwaka 2009 zilitoa mamlaka hayo kwa Waziri na kwa Mkurugenzi wa Mazingira. **Katika Kanuni mpya za mwaka 2019, mamlaka ya kutoa vibali yamebaki kwa Waziri mwenye dhamana ya mazingira tu akishauriwa na Mkurugenzi wa Mazingira.**

Kanuni za mwaka 2009 hazikumtambua *Export Controller* kama mamlaka yake yanavyoelekezwa chini ya Sheria "*the Export Control Act*" inayosimamiwa na Wizara ya Viwanda na Biashara katika usimamizi wa usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi. Hali hii imezingatiwa katika kanuni za 2019 ambapo *Export Controller* atapewa nakala ya kibali kilichotolewa na Waziri pamoja na nyaraka nyingine ili aweze kutoa leseni ya kusafirisha bidhaa nje ya nchi kwa mujibu wa *The Export Control Act*.

Kanuni mpya za mwaka 2019 zimeandaliwa kwa kuzingatia Makundi ya aina za Taka Hatarishi kulingana na Mkataba wa Basel unaohusu Udhibiti wa Usafirishaji na Utupaji wa Taka Hatarishi baina ya Nchi na Nchi ambapo Tanzania ni nchi mwanachama wa Mkataba huo. Kwa kuwa mwanachama wa Mkataba huu, nchi yetu inashirikiana na nchi wanachama wengine kudhibiti taka hatarishi zinazovuka mipaka.

Kanuni za mwaka 2009 hazikuweka bayana masharti ya kuzingatiwa na mmiliki wa kibali. Suala hili limezingatiwa katika Kanuni mpya za mwaka 2019. Uwepo wa masharti ya mmiliki wa kibali kutarahisisha ufuatiliaji wa uzingatiaji wa masharti yaliyoainishwa katika kibali cha usimamizi wa taka hatarishi pamoja na masuala ya hifadhi na usimamizi wa mazingira kwa ujumla wake.

***Inaendelea Uk. 10***

***Inatoka Uk. 9***

Kanuni za mwaka 2009 hazikuweka bayana majukumu ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) ya kushughulikia maombi ya vibali kama sehemu ya Mamlaka yake ya kusimamia uzingatiaji na utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Ma ingira na Kanuni zake. Suala hili limezingatiwa katika Kanuni mpya za mwaka 2019 kwa kuzingatia jukumu hilo kwa NEMC. Kanuni hizi mpya zitarahisisha utaratibu wa kushughulikia maombi kwa kuzingatia kwamba ofisi za kanda za NEMC zipo mikoa saba ambayo ni pamoja na mikoa ya Arusha, Dodoma, Mbeya, Mwanza, Dar es salaam, Kigoma na Mtwara. Ofisi zitapokea maombi na kuyafanyia kazi na hatimaye kutoa mapendekezo kwa Waziri, kupitia Mkurugenzi wa Mazingira kwa ajili ya idhini na kutoa kibali.

Kanuni mpya za mwaka 2019, zimeainisha aina ya shughuli za usimamizi wa taka hatarishi ambazo zinapaswa kuwa na kibali cha Waziri mwenye dhamana ya Mazingira. Shughuli zinazopaswa kuombewa kibali ndani ya nchi ziko nne ambazo ni kukusanya, kutunza, kusafirisha, na kumiliki au kuendesha mtambo wa usimamizi wa taka hatarishi. Aidha, shughuli za usafirishaji nje ya nchi, kuingiza au kupitisha nchini taka hatarishi zinapaswa kuombewa kibali ambacho pia hutolewa na Waziri husika.

Kanuni za mwaka 2019, zimeelekeza kuwa shehena yoyote ya taka hatarishi itakayoingizwa au kupitishwa nchini bila kufuata masharti ya Kanuni hizi, **itachukuliwa kuwa ni usafirishaji haramu wa taka hatarishi** (*illegal traffic*) na zinapaswa kurejeshwa katika nchi zilikotoka kwa gharama za msafirishaji.

Kanuni za mwaka 2019 zimeweka adhabu kali zaidi ukilinganisha na Kanuni za mwaka 2009 kwa makosa ya kutokuwa na kibali cha kusimamia taka hatarishi nchini. Adhabu hizo ni faini kuanzia **milioni tano hadi bilioni kumi au kifungo kisichozidi miaka kumi na mbili au vyote kwa pamoja.**

**Ndugu Wananchi**, Ofisi ya Makamu wa Rais imefanyia pia marekebisho ya Kanuni za Ada na Tozo za Usimamizi wa Mazingira za Mwaka 2008. Ambapo kwa upande wa Taka Hatarishi Ada na Tozo zimepungua kwa viwango tofauti kulingana na aina ya taka na uzito kwa tani, punguzo hilo linaanzia Tsh milioni moja na nusu mpaka milioni tano.

Aidha, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na wadau imeaandaa Kanuni mpya za Udhibiti na Usimamizi wa Taka za Kielektroniki za Mwaka 2019. Awali udhibiti na usimamizi wa taka hizi ulikuwa chini ya Kanuni za Udhibiti na Usimamizi wa Taka Hatarishi. Hatua hii ya kuandaa Kanuni mahsusi za udhibiti wa taka za kielekroniki imetokana na changamoto ya kuongezeka kwa taka za kielekroniki kwa kasi kubwa ambapo hali hii inachangiwa na ongezeko la matumizi ya vifaa vya kielektroniki. Kutokana na hali hiyo ilionekana ni vyema tukaweka mfumo mahsusi wa kusimamia taka za aina hii kwa kuwa na Kanuni maalum ambazo tayari nazo zimekwishaanza kutumika.

Ikumbukwe pia kampuni zinazojishughulisha na biashara ya taka za kielektroniki zitatakiwa kuwa na kibali kinachotolewa na Waziri mwenye dhamana ya Mazingira.

***Inaendelea Uk. 10***

*Inatoka Uk. 10*

Vile vile, kwa mujibu wa Kanuni za Ada na Tozo za Usimamizi wa Mazingira za Mwaka 2019, kampuni hizo zitatakiwa kulipa Ada na Tozo kati ya shilingi milioni moja na nusu hadi shilingi milioni tano.

**Ndugu wananchi**, nitoe rai kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia Halmashauri zote nchini zifuatilie watu binafsi, Kampuni na Viwanda kuhakikisha kuwa Sheria na Kanuni za Udhibiti wa taka hatarishi zinazingatiwa ipasavyo hali ambayo itachangia katika udhibiti wa uchafuzi wa mazingira.

**Ndugu wananchi,**

Napenda kusisitiza kuwa, hatua hii iliyochukuliwa na Ofisi ya Makamu wa Rais ya kufanya marekebisho katika Kanuni hizi na kuweka mfumo bora wa kisheria wa kusimamia taka hatarishi inalenga sio tu kuhakikisha kuwa mazingira yanalindwa na kusimamiwa bali pia miundombinu ya nchi inalindwa ipasavyo. Kama tunavyofahamu, mojawapo ya taka hatarishi ni chuma chakavu, kuna baadhi ya wafanyabiashara na watu ambao sio waaminifu wanafanya biashara hii bila kuwa na vibali husika, lakini pia wapo ambao wana vibali lakini hawafuati masharti yaliyowekwa chini ya vibali hivyo. Moja ya sharti muhimu ni kwamba kila mwenye kibali cha chuma chakavu anapaswa kutoa taarifa ya chanzo cha chuma chakavu hicho na mahali anapokipeleka. Na hiyo inafanyika kwa kujaza 'tracking form' namba 3, **kutokufanya hivyo ni kosa kubwa chini ya Kanuni hizi**. Adhabu kwa makosa kama haya ni kama nilivyotamka hapo awali ambayo ni faini kuanzia **Shilingi milioni tano hadi bilioni kumi au kifungo kisichozidi miaka kumi na mbili au vyote kwa pamoja.**

Aidha, wapo baadhi ya watu ambao wamekuwa kwa makusudi wakihujumu miundombinu ya umma na watu binafsi na kwenda kuuza kama chuma chakavu. Wapo pia wengine ambao wanakwepa kulipa kodi stahiki kwa Serikali. **Niwatake kuacha udanganyifu huo kwa kuwa sasa tumeweka mfumo wa kiutawala, kisheria na kikanuni ambao sio rahisi kufanya udanganyifu huo tena bila kugundulika.** Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) tumejipanga kusimamia Kanuni hizi ipasavyo.

Niombe pia Mamlaka nyingine vikiwemo Vyombo vya Ulinzi na Usalama, Mamlaka ya Mapato, Mamlaka ya Bandari na wadau wote tushirikiane kuhakikisha kuwa sheria zetu zinasimamiwa ipasavyo.

**Mwisho,**

Natoa rai kwa wananchi na wafanya biashara wanaojihusisha na biashara ya taka hatarishi hususan chuma chakavu hapa nchini kuzingatia mambo ya msingi yaliyoanishwa katika kanuni hizi mpya. Kanuni hizi zinapatikana katika Tovuti ya Ofisi ya Makamu wa Rais ambayo ni www.vpo.go.tz na ile ya NEMC ambayo ni www.nemc.or.tz

Imetolewa na:

George B. Simbachawene (Mb.)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA)**

23 DESEMBA, 2019

# Waziri Simbachawene aipa kibarua Idara ya Mazingira

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. George Simbachawene ameielekeza Idara ya Mazingira kufanya utafiti katika vijiji vya Nyabu na Chipogoro wilayani Mpwapwa mkoani Dodoma na kuja na mkakati wa kuhakikisha mafuriko yanadhibitiwa.

Simbachawene ametoa maelekezo hayo leo Desemba 7, 2019 wakati wa ziara ya kikazi ya kukagua athari za mafuriko katika vijiji hivyo kwenye Kata ya Chipogolo yaliyotokea hivi karibuni na kusababisha kifo na kaya kadhaa kukosa makazi.

Akizungumza na wananchi wa vijiji hivyo alisema unahitajika mpango mkakati wa kimazingira na mkono wa Serikali kupitia mamlaka zake mbalimbali kwa pamoja ili kunusuru vijiji hivyo na athari za mafuriko yanayokea

Aidha Simbachawene ambaye pia ni mbunge wa Kibakwe alikemea tabia ya baadhi ya wananchi kukata miti hasa katika maeneo ya kwenye milima vitendo vinavyochangia mmomonyoko wa udongo na hivyo maji kutiririka kwa kasi na kusababisha mafuriko.

“Ndugu zangu hizi mvua zinazonyesha si kwamba ni kubwa sana kuliko za miaka iliyopita ni za kawaida na haya mafuriko hayatokani na mvua iliyonyesha eneo hili yametoka kwenye miinuko kule watu walikokata miti, kwa hiyo nawaomba mshirikiane na Serikali mtoe taarifa za wanaokata miti,” alisema.

Waziri Simbachawene aliongeza kuwa jukumu la kila mwananchi ni kupanda miti na kusisitiza viandaliwe vitalu vya miche ya miti kwa ajili ya kupanda ili kupunguza kasi ya maji yanayotiririka kutoka kwenye miinuko.

Katika ziara hiyo pamoja na mambo kadhaa pia aliitembelea familia ya kijana aliyefariki katika mafuriko hayo yaliyotokea kati ya Novemba 28 hadi 30 mwaka huu na kuathiri vijiji hivyo.

Pia alitembelea majengo yaliyoathiriwa na mafuriko yakiwemo zahanati, kituo cha Polisi, msikitiki na makazi ya wananchi katika vijiji vya Chipogoro na Nyabu wilayani humo.

Kwa upande wake Mtendaji wa Kata ya Kijiji cha Nyabu Yona Mganga wakati akisoma taarifa ya tukio hilo alisema mafuriko hayo yameleta madhara mbalimbali yakiwemo kupoteza maisha kwa mtu mmoja, nyumba kubomoka na kusababisha watu kukosa makazi.

Pia alisema miundombinu ya barabara kuu ya kwenda Iringa kutopitika kwa saa kadhaa kulikotokana na kujaa kwa maji barabarani na huvyo magari kushindwa kusogea.



***Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. George Simbachawene (kulia) akikagua majengo mbalimbali yaliyoathiriwa na mafuriko katika kijiji cha Chipogoro Jimbo la Kibakwe wilayani Mpwapwa mkoani Dodoma alipofanya ziara ya kikazi.***

# HABARI PICHA



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Suluhu Hassan akiweka Shada la Maua kwenye Mnara wa kumbukumbu Eneo waklipoozikwa Wahanga wa Ajali ya Kivuko cha MV Nyerere Kisiwani Ukara Wilayani Ukerewe alipotembekea Eneo hilo.*

*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. George Simbachawene akitoa maelekezo kwa wataalamu alipotembelea zahanati ya Chipogoro Jimbo la Kibakwe wilayani Mpwapwa mkoani Dodoma ambayo iliathiriwa na mafuriko hivi karibuni.*





*Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Mhandisi Joseph Malongo (aliyeshika bendera) akiwa katika maadhimisho ya miaka 58 ya Uhuru wa Tanganyika yaliyofanyika katika Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.*



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akipokea Saluti ya heshima kutoka kwa Jeshi Usu la Maliasili wakati wa Maadhimisho ya Miaka 60 ya kuanzishwa kwa Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) yaliyofanyika Eneo la Fort Ikoma Serengeti, Mara..*

# Tunawatakia Heri ya Mwaka Mpya 2020


**LIMETOLEWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

S.L.P. 2502, DODOMA, TANZANIA
Simu: +255 266 235 2038
Nukushi: +255 266 235 0002
Baruapepe: ps@vpo.go.tz
Tovuti: www.vpo.go.tz